Wito Kwa Waislamu Kuuendea Ukweli

Shaykh Muslim Bhanji

Al-Islam.org

Author(s):

Shaykh Muslim Bhanji [3]

Makala haya yanaeleza kwa kina kuwa mrithi wa haki wa Mtume (s.a.w.w.) baada yake ni nani na dalili zote zime tolewa kutoka vitabu vya Sahihi na vinavyo tegemewa na kurejewa.

Category:

Imam Ali [4]
Sunni & Shi'a [5]
Hadith Sciences [6]

Miscellaneous information:
Wito Kwa Waislamu Kuuendea Ukweli Sheikh Muslim Bhanji Tanzania Ithna Ashariyah Community (T.I.C.)

Featured Category:

Shi'a beliefs explained [7]

Bismihi Ta'ala
***"Na katika haya imekujia Haki na mauidha na ukumbusho kwa wale wanaoamini."*(*Suratul Hud 11:120*)**

Utangulizi

Tofauti kubwa iliyopo baina ya Waislamu wa Kishia na Waislamu wa Kisunni ni juu ya imani ya Ukhalifa na Uimamu baada ya kuondoka kwa Mtukufu *Mtume Muhammad* (*s.a.w.w*). Sisi waislamu wa Kishia tunaamini kuwa Imam *Ali bin Abi Talib* (*a.s*) ni khalifa na Imam wa kwanza baada ya Mtume (s.a.w.w.) ambapo ndugu zetu Waislamu wa Kisunni wanaamini kwamba *Seyidina Abubakar* (*r.a.*) alikuwa ni khalifa wa kwanza.

Ingawa kuna tofauti nyingine ndogo ndogo zilizopo baina ya madhehebu makubwa ya Uislamu (Shia na Sunni) kwa mfano katika sheria (Fiqh) kama vile kukunja mikono wakati wa kusali au kuinyoosha n.k. lakini hizi ni tofauti ndogo ndogo sana ambazo zinaweza hata kupatikana ndani ya madhehebu manne ya Kisunni (*Imam Shafi, Maliki, Hanafi na Hanbali*). Masuala haya tutayajadili hapo baadaye InshaAllah.

Mbali na tofauti hiyo kubwa kuna mambo yanayofanana katika imani za Waislamu wa Shia Ithna Ashariya na Waislamu wa Kisunni. La kwanza ni nguzo tano za Uislamu, yaani :

(a) Shahaada – Laa Ilaaha Illallah – Muhammadur Rasuulullah – Hakuna mungu apasaye kuabudiwa

kwa haki isipokuwa Allah – na Muhammad ni Mtume wa mwisho wa Allah.
(b) Sala tano za kila siku
(c) Kufunga mwezi wa Ramadhan
(d) Kuhiji katika nyumba takatifu ya Kaa'ba
(e) Zakat kwa ajili ya maskini

Kwa pamoja Shia Ithna Asheriyya na Sunni wanaamini juu ya kitabu cha mwisho cha Allah Qur'an kuwa bado kipo vile vile bila mapunguzo au maongezo, na wanajaribu kufuata maamrisho yake bila kubakiza.

Kwa pamoja Shia Ithna Asheriya na Sunni wanaichukulia Sunnah na Siira ya Mtume kuwa ni muongozo kwa Waislamu katika maisha yao ya kila siku na wanajaribu kuifuata kwa uangalifu mkubwa ili wapate kuokoka hapa duniani na Akhera.

Ingawa wapo watu waharibifu katika jamii ambao kwa makosa wanatushutumu sisi Shia Ithna Asheriya kwa madai mbalimbali ya uongo kama vile kudai kuwa Shia wana Qur'an yao au madai kuwa eti Shia wanaamini juu ya Utume wa Imam *Ali bin Abitalib*, n.k. Wale wote wanaoutafuta ukweli, wanatakiwa kuyatupilia mbali madai (shutuma) haya maovu dhidi yetu na tunawaomba watembelee misikiti na madrasah zetu ambazo mara zote zipo wazi kwa Mwislamu yeyote kuja kuthibitisha imani zetu.

Kuna Shia zaidi ya millioni 250 duniani kote ambao wanaamini kuwa Mtume Muhammad (s.a.w.w.) ni Mtume wa mwisho na wanafuata maamrisho ya Qur'an na Sunna za Mtume (s.a.w.w.) katika maisha yao ya kila siku. Katika manispaa ya Dodoma peke yake, sisi Shia tuna misikiti miwili; ***Khoja Shia Masjid na Masjid Imam Mahdi*** (a.s) na tunawaalika waumini wote wa Kiislamu kututembelea katika misikiti hii ili kupata ushahidi kwa macho yao kuhusiana na imani na matendo yetu kabla ya kuangukia katika mtego wa waharibifu wanaotuzulia habari za uongo.

Kwa Nini Shia Wanaamini Kuwa Imam Ali Ni Khalifa Wa Kwanza Baada Ya Mtume ?

Shia Ithna Ashariya wanaamini kuwa Imam *Ali bin Abitalib* ni Khalifa na Imam wa kwanza baada ya Mtume (s.a.w.w.) kwa kuzingatia sababu moja rahisi sana na iliyo wazi. Sababu hii ni kuwa; *"Imam Ali bin Abitalib (a.s) aliteuliwa kwa amri ya Mwenyezi Mungu kuwa Khalifa wa kwanza wa Waislamu na Mtume mwenyewe kwa amri ya Mwenyezi Mungu (s.wt).* Hii ndio sababu na hakuna sababu nyingine.

Katika Qur'an tukufu (59: 7) Mwenyezi Mungu anasema: "-----Na anachokupeni Mtume basi pokeeni na anachokukatazeni jiepusheni nacho". Qur'an (33:36):

"Na haiwi kwa wanamume aliyeamini wala kwa mwanamke aliyeamini, Mwenyezi Mungu na Mtume wake wanapokata shauri, wawe na hiari katika shauri lao. Na mwenye kumuasi Mwenyezi Mungu na Mtume wake, hakika amepotea upotevu ulio wazi".

Shia wanaamini kwamba maadamu Mtume (s.a.w.w.) mwenyewe kwa amri ya Mwenyezi Mungu alimteua *Imam Ali* (*a.s*) *kuwa Khalifa*, Waislamu hawana hiari yoyote isipokuwa kutii amri hii.

Mitume Na Maimamu Huteuliwa Na Mwenyezi Mungu Tu Na Si Vinginevyo

Shia wanaamini kuwa ni Mwenyezi Mungu (Allah) tu ndiye anayeweza kumteua mrithi wa Mtume na Imam wa Waislamu, na kwamba Ummah wa Kiislamu hauna hiari yoyote katika jambo hili.

Ushahidi Kutoka Katika Qur'an

Aya za *Qur'an* zifuatazo zina thibitisha kuwa Mitume wote na Maimamu waliteuliwa na Allah Mwenyewe.

1) ***"Na Mola wako huumba atakavyo na huchagua; Hawana hiari ya kuchagua".*** (***Qasas 28:68***)

2) ***"Mimi nitaleta khalifa katika ardhi".*** (***Baqara 3:30***)

3) ***"Ewe Daud! Hakika tumekujaalia kuwa khalifa katika ardhi..... ".***
(***Saad 38 :26***)

4) ***"(Allah) alisema kwa hakika nitakufanya wewe (Ibrahimu) kuwa Imam wa watu (Ibrahimu); alisema Je, na katika kizazi changu pia? Akasema (Ndio lakini) ahadi yangu haitawafikia waovu (madhalimu)".*** (***Baqara 2:124***)

5) ***"Na tukawajaalia kuwa Maimamu wanaoongoza kwa amri Yetu".***
(***Anbiya 21:73***)

6) ***"Na Unifanyie Waziri (msaidizi) katika jamaa zangu ..... ndugu yangu Haruni ..... Mwenyezi Mungu Akasema: Hakika umepewa maombi yako, ewe Musa".***
(***Taha 20: 29 – 36***)

7) ***"Na hakika Mwenyezi Mungu alimchagua Adamu na Nuhu na kizazi cha Ibrahimu na kizazi cha Imrani juu ya walimwengu wote. Ni kizazi cha wao kwa wao; na Mwenyezi Mungu ni Mwenye kusikia na Mwenyekujua".***
(***Ale Imran 3:33 – 34***).

8) ***"Mwenyezi Mungu amemchagua (Taluti) juu yenu na amemzidishia wasaa wa elimu na kiwiliwili, na Mwenyezi Mungu ni Mwenye wasaa na Mwenye kujua".*** (***Baqara 2:247***)

9) ***"Akasema (Allah) : Ewe Musa! Mimi nimekuchagua juu ya watu wote kwa ujumbe wangu na kwa kusema nawe kwangu, basi pokea haya niliyokupa na uwe miongoni mwa wanao shukuru".***
(***A'raaf 7:144***)

10) ***"Na tukawafanya miongoni mwao Maimamu wanaoongoza kwa amri yetu, waliposubiri na walikuwa wakiyakinisha aya zetu"***. (***Sajdah 32: 24***).

Aya zote za Qur'an zilizotajwa hapo juu na nyingine nyingi ambazo hatukuzitaja zinathibitisha kwamba Mitume wote na warithi wao waliteuliwa moja kwa moja na Mwenyezi Mungu bila hiari ya Ummah.

Ushahidi / Uthibitisho Wa Kiakili Na Kihistoria

1) **Ada Ya Mitume Waliotangulia**: Ada ya Mitume wote ilikuwa ni kuteua warithi wao kwa amri ya Allah bila kuingiliwa na Ummah. Historia ya Mitume hawa haitoi mfano hata mmoja wa mrithi wa Mitume aliyechaguliwa kwa kura za wafuasi wake. Hakuna sababu kwa nini linapokuja suala la mrithi wa Mtume wa Mwisho, Muhammad (s.a.w.w.) sheria na kanuni hii ya Mwenyezi Mungu ibadilishwe.

Mwenyezi Mungu anasema: ***"Wala hutapata mabadiliko katika kawaida ya Mwenyezi Mungu (Mwendo Wake)".*** (***Ahzab 33: 62***)

2) **Mifano Wa Warithi Wa Mitume Waliopita**: Baadhi ya mifano ya warithi wa mitume walioteuliwa na Mitume waliopita kwa amri ya Mwenyezi Mungu (s.w.t).

a) ***Nabii Adamu alimteua Shiith***

b) ***Nabii Ibrahim alimteua Ismail***

c) ***Nabii Ya'qub alimteua Yusuf***

d) ***Nabii Musa alimteua Yusho' bin Nuun***

e) ***Nabii Issa alimteua Sham'uun***

f) ***Nabii Muhammad (s.a.w.w.) alimteua Imam Ali Ibn Abi Talib***

Qur'an inasema: ***"Na wakumbuke waja wetu Ibrahim na Is-haq na Ya'qkub waliokuwa wenye nguvu na busara. Hakika sisi tuliwachagua kwa lile jambo zuri kabisa la kuikumbuka Akhera. Na bila shaka walikuwa mbele yetu ni miongoni wa watu bora waliochaguliwa. Na mkumbuke Ismaili na Al-Yasaa na Dhulkifli; na hao wote walikwa miongoni mwa watu bora".*** (***Saad 38:45 - 48***).

Qur'an inasema: ***"Na hizi ndizo hoja zetu tulizompa Ibrahim juu ya watu wake. Tunamnyanyua katika vyeo yule tumtakaye. Hakika mola wako ndiye Mwenye hikima na ndiye ajuaye, Na tukampa (Ibrahim) Is-haq na Ya'quub, wote tukawaongoa. Na Nuhu tulimwongoa zamani. Na katika kizazi chake Daudi na Suleimani na Ayyub na Yusuf na Musa na Haruni. Na hivi ndivyo tuwalipavyo wafanyao mema. Na tukamwongoza Zakaria na Yahya na Issa na Ilyasi wote (walikuwa) miongoni mwa watu wema. Na (tukamwongoza) Ismail na Al-Yasaa (Ilisha) na Yunusi na Luti. Na wote tukawafadhilisha juu ya walimwengu. Na (tukawaongoa) baadhi ya baba zao na vizazi vyao na ndugu zao. Na tukawachagua na kuwaongoza katika njia iliyonyooka. Huu ni uongozi wa Mwenyezi Mungu. Kwa huo humwongoza amtakaye katika watu wake".*** (***An-aam 6:83 - 88***).

3) **Mtume Hakufariki Kabla Ya Kumteua Mrithi Wake (Wasii Wake)**: Mitume wote waliopita pamoja na *Mtume Muhammad* (*s.a.w.w.*) hawakupata kuziacha Ummah zao japo kwa muda mfupi bila kuacha watu watakaoshika mahala pao (warithi). Hata walipokuwa wanatoka kwa safari fupi walikuwa wanaacha watu wa kushika mahala pao (warithi). Je, inawezekana kwa *Mtume Muhammad* (*s.a.w.w.*) kuondoka na kuuacha Ummah wake bila Wasiy (Mrithi).

Mtume Muhammad alikuwa anajua kuwa muda wake wa kuondoka duniani umekaribia, alijua kuwepo kwa wanafiki katika jamii ya waislam, alijua kuwepo kwa watu walioendekeza tamaa ya madaraka katika mioyo yao, hivyo asingeweza kuuacha Ummah wake bila wasii (mtu atakayeshika mahala pake). Alimteua *Imam Ali bin Abitalib* kwa amri ya Mwenyezi Mungu kuwa mrithi na mtu atakayeshika mahala pake baada ya kuondoka kwake hapa Duniani.

4) Sababu zinazofanya ulazima wa Mitume kuteuliwa na Mwenyezi Mungu ni hizo hizo zinazofanya ulazima wa Wasii, *Imamu na Khalifa* kuteuliwa na Mwenyezi Mungu kwa sababu wote wanateuliwa kufanya kazi za Allah.

5) Ikiwa *Imam au Khalifa* atateuliwa au kuchaguliwa na watu, utii wake wa kwanza hautakuwa kwa Mwenyezi Mungu bali kwa watu waliomchagua. Kwa sababu msingi wa mamlaka yake itakuwa ni watu, mara zote atajaribu kuwaridhisha watu, vinginevyo ikiwa watapoteza imani juu yake, atapoteza nafasi yake. Mtu wa aina hii hataweza kutekeleza majukumu ya dini bila woga au upendeleo, na macho yake daima yatakuwa katika mtazamo wa kisiasa.

6) Historia ya Uislamu ina mifano tele ya maovu yaliyofanywa na makhalifa walioteuliwa na wanadamu. Mfano bora kabisa ni ule wa *Yazid bin Muawiya bin Abu Sufiyan* ambaye waziwazi kabisa alizipuuza sheria, alikunywa pombe kweupe, alimuua mjukuu wa Mtume *Imam Husayn* (*a.s*) na alituma jeshi Makka ambalo liliichoma nyumba tukufu ya Al-Ka'aba na kufanya maovu mengine mengi. (*Tazama Taarikhul Khulafaa na Suyuti*).

7) Pia ni Mwenyezi Mungu tu ndiye anayejua hisia na mawazo ya ndani ya wanaadamu, hakuna mwingine anayeweza kujua undani wa mtu mwingine. Wakati fulani anaweza kujifanya ni mcha Mungu na mwenye kumuogopa Mwenyezi Mungu ili tu kuwaonyesha wenzake au ili apate umaarufu ili achaguliwe na wenzake kuwa kiongozi kwa manufaa ya kiulimwengu.

Mifano ya aina hii si haba katika historia. Tuchukue mfano wa *Khalifa Abdul Malik bin Marwan* ambaye alikuwa anamaliza siku nzima msikitini akisali na kusoma Qur'an. Siku moja aliarifiwa juu ya kifo cha baba yake na kwamba watu walikuwa wanamsubiri ili watoe kiapo cha utii kwake. Aliifunika Qur'an na kusema : *"Huku ndio kuachana kwangu mimi na wewe* (*Qur'an*)*".* (Yaani kupata Ukhalifa ndio mwisho wa kusoma Qur'an). (*Tazama Taarikhul Khulafaa ya Suyuti, Ukurasa 217*). Sifa muhimu za Imam ni Mwenyezi Mungu tu ndiye anayezijua.

8) **Ma'asum** – Kwa mujibu wa Shia, Maimamu na Makhalifa lazima wawe Ma'asum – yaani waliotakasika kutokana na madhambi na uchafu. Hivyo Maimamu wote 12 walioteuliwa na Mtume Muhammad

(s.a.w.w.)walikuwa Ma'asum (wasio na madhambi), na historia ya Uislamu inashuhudia uma'asumu, ucha Mungu, elimu na tabia njema za Maimamu 12 wa Shia Ithna Ashariyah, wa kwanza wao akiwa Imam Ali bin Abitalib (a.s). Mada hii itajadili zaidi katika makala yajayo.

Ismah (kutakasika kutokana na madhambi) ni sifa kutoka kwa Mungu ambayo haiwezi kupatikana kwa jitihada ya mtu tu bila ridhaa ya Allah, hivyo Maimamu wanatakiwa wateuliwe na Allah tu. Sababu zote zinazothibitisha kuwa Mitume lazima wawe Ma'asum pia hizo hizo zinathibitisha kuwa Maimamu ni Ma'asum. Maelezo zaidi yatafuatia.

9) **Miujiza** – Kwa mujibu wa Shia, Maimamu walioteuliwa na Allah lazima wawe na uwezo kutoka kwa Allah wa kuonyesha miujiza kila itakapohitajika ili kuthibisha Uimamu wao kama walivyokuwa wakifanya Mitume. Historia ya Uislamu inathibitisha tena kuwa Maimamu 12 walioteuliwa na Allah walionyesha miujiza na waliwashinda maadui zao katika swala la ukweli (haki). Makhalifa walioteuliwa na watu huwa hawana uwezo wa kuonyesha miujiza, jambo ambalo ni muhimu sana kwa Mitume na Maimamu.

10) **Ubora** – Shia wanaamini kuwa, kama ilivyo kwa Mtume, Imamu lazima awazidi wale wote anaowaongoza katika sifa bora kama vile elimu, Ushujaa, Ujasiri, Ucha Mungu, na Ukarimu. Lazima awe na elimu kamili ya sheria za Mwenyezi Mungu. Hapa pia, sifa hizi hazipatikani kwa Khalifa yeyote aliyechaguliwa au kuteuliwa na watu isipokuwa kwa Maimamu 12 wa Shia Ithna Ashariya walioteuliwa na Allah. Soma makala yatakayofuata kwa maelezo zaidi.

Pointi zote hizi zinathibitisha waziwazi kuwa warithi, Makhalifa na Maimamu wa Mitume wote lazima wateuliwe na Allah tu. Maovu yote, kutokuwepo kwa Umoja, Ujinga, Uvunjaji wa sheria za kiislamu n.k. yote haya yanatokana na makhalifa waliochaguliwa na watu waliopinga amri ya Allah kupitia kwa Mitume wake kuhusiana na suala la ukhalifa.

Ili kupata uokovu, ukweli na utukufu waislamu wanatakiwa warudi na kufuata amri ya Allah (s.w.t) kuhusiana na suala la Imam baada ya Mtume, tunawaita katika ukweli na haki. Lakini ni lini Mtume Muhammad (s.a.w.w.) alimteua Imam Ali bin Abi Talib (a.s) kuwa Khalifa na Imam? Je, kuna ushahidi wowote katika Qur'an tukufu, Sunnah na historia ya Uislamu unaothibitisha uteuzi huu?

Ili kupata majibu ya maswali haya soma makala Na. 2.

Sheikh Muslim Bhanji
Tanzania Ithna Ashariyah Community (T.I.C.)
Dodoma.
June 2001

Bismihi Ta'ala
"Na katika haya imekujia Haki na mauidha na ukumbusho kwa wale wanaoamini." (***Suratul Hud 11:120***)

Katika makala yetu Na. 1 tumeonyesha waziwazi kabisa kuwa Mitume wote waliopita pamoja na mawasii, warithi na makhalifa wao wote waliteuliwa na Allah (s.w.t) tu, na mamlaka haya ya kumchagua Mtume au Khalifa hakupewa mtu yeyote katika Ummah.

Kama ilivyokuwa kwa mitume wote waliotangulia Mtume Muhammad (s.a.w.w.) pia kwa amri ya Mwenyezi Mungu (s.w.t) alimteua Imam Ali bin Abitalib (a.s) kuwa Wasii na Imam na Khalifa wa Ummah wa Kiislamu baada yake. Alhamdullilah, sisi Shia Ithna Ashariyah tunatii amri hii ya Allah (s.w.t) kama amri iliyo juu yetu na tunaamini kwa dhati kuwa Imam Ali bin Abitalib (a.s) ni Khalifa wa kwanza wa Ummah wa Kiislamu.

Katika hii makala na. 2, tutaonyesha baadhi ya ushahidi kutoka katika Qur'an tukufu, Sunnah na Hadithi za Mtume Muhammad (s.a.w.w.)na kutoka katika Historia ya Uislamu, ushahidi ambao utathibitisha bila kuacha chembe ya shaka kuwa Mtume Muhammad (s.a.w.w.) hakumteua yeyote isipokuwa *Ali bin Abitalib* kuwa wasiy baada yake.

Waislamu wengi na maulamaa wakubwa wa *Ahlul Sunnah Wal Jama'ah* baada ya kuujua ukweli huu walibadili na kuwa wafuasi wa madhehebu ya Kiislamu ya Shia Ithna Ashariya na sasa wanaamini kwa dhati kabisa kuwa *Imam Ali bin Abitalib* ni Khalifa wa kwanza wa Waislamu baada ya Mtume Muhammad (s.a.w.w.). Maelfu ya Waislamu kila mwaka wanaikubali (wanaifuata) njia ya haki, njia iliyonyooka baada ya kufanya utafiti na baadhi yao wameandika pia vitabu juu ya utafiti wao. Baadhi ya mifano ya Wanazuoni wa Kisunni walioingia katika madhehebu ya Shia Ithna Ashariya na wakaandika vitabu juu ya utafiti wao ni :

a) ***Sheikh Muhammad Samawi Tijani wa Tunisia*** ambaye baada ya kuwa Shia, aliandika vitabu kama vile: *"Hatimaye Nimeongoka", "Shia ni Wafuasi Halisi wa Sunna ya Mtume", "Waulize Wale Wanaojua", "Kuwa Pamoja na Wakweli",* n.k.

b) ***Sheikh Muhammad Mar'iy Al-Amin Al-Antaaqi wa Uturuki*** ambaye aliandika kitabu chenye kurasa 520 chenye jina *"Kwa nini nilichagua madhehebu ya Shia - Madhehebu ya Ahlul-Bait* (*a.s*)*?"*

c) ***Molwi Sheikh Hafidh Ali Muhammad Fathuddin Al-Hanafi*** aliyeandika kitabu *"Fulkun Najaat Fil Imamah Wa-Salah"* (*Safina ya wokovu katika Uimamu na Sala*)*.* Kitabu hiki chenye kurasa 328 kinathibitisha Uimamu wa Ali bin Abitalib na jinsi Mtume (s.a.w.w.) alivyokuwa akisali.

d) ***Profesa Harun Abdallah wa Nigeria a***mbaye ana *Shahada ya juu katika Uhandisi wa Madini* (*Mining engineering*)*,* alifanya utafiti wa kina na aliridhika kuwa madhehebu ya Shia Ithna Ashariya ni ya kweli. Aliandika kitabu juu ya utafiti wake *"The Missing Link"* ambacho kina kurasa 387.

Wapendwa wasomaji, tuna uhakika kwamba baada ya kusoma makala haya na makala yatakayofuatia, mkiwa bila upendeleo akilini na ugumu wa kubadilika kutokana na mazoea na uzoefu wa nyuma, mtaukubali ukweli, na kuamini kuwa wafuasi wa madhehebu ya Ahlulbait ya Kishia wako katika njia iliyonyooka, wale ambao Mtume (s.a.w.w.) aliwatabiri: *"Umma wangu baada yangu utagawanyika katika*

makundi 73 na wote watakuwa watu wa motoni isipokuwa kundi moja". (*Al-Mustadrak ya Hakimu, Juzuu 1, Uk. 128; Sunan Abi Dawood, Juz. 4, Uk. 198*; *Sunan Ibn Maajah, Juz. 2, uk. 1321*).

Wapendwa wasomaji, tunawaita katika njia iliyonyooka madhehebu ya Shia Ithna Ashariya, madhehebu ya Ahlul Bayt (a.s) na jiokoeni kutoka katika moto wa Jahanamu. Tafadhali jisikie huru kuja kututembelea na kuomba ushahidi na vitabu zaidi vya rejea. Waislamu walio wengi wanafuata madhehebu ya mashehe wao na babu zao kibubusa bila kuwa na ushahidi wowote, kama ilivyo kwa wasio Waislamu wanavyofuata dini za babu zao kibubusa. Qur'an Tukufu imewalaumu watu wa aina hii ambao hawafanyi utafiti ili kutafuta ukweli:

"Na wanapoambiwa Fuateni aliyoyateremsha Mwenyezi Mungu, husema: Bali tutafuata yale tuliyowakuta nayo baba zetu. Je, hata kama baba zao walikuwa hawafahamu chochote wala hawakuongoka?" (***Baqara 2:170***).

Uthibitisho / Ushahidi Kwamba Imam Ali Ni Khalifa Wa Kwanza

Ni ukweli unaoeleweka wazi duniani kote kwamba kama unataka kumshawishi mtu kuuendea ukweli wa imani yako, na ikiwa mtu mwenyewe hakubaliani na imani yako, inabidi utumie mantiki na vitabu vyake yeye mwenyewe anavyovikubali. Kwa mfano kama unataka kumshawishi Mkristo juu ya Utume wa Nabii Muhammad (s.a.w.w.) inabidi umshawishi kwa kutumia ushahidi ulio katika kitabu chake anachokiamini: Biblia Takatifu.

Halikadhalika tutatoa ushahidi kuthibitisha kuwa Mtume Muhammad (s.a.w.w.) alimteua Imam Ali (a.s) kwa amri ya Allah (s.w.t) kuwa wasii wake, kutoka katika Qur'an Tukufu na vitabu vya Tafsiir, vitabu vya Siirah, vitabu vya Tarikh (Historia), na vitabu vya Hadithi vilivyoandikwa na Maulamaa wa Kisunni wao wenyewe.

Ushahidi Na. 1 : Hadithul Indhaar au Da'wat Dhul Ashirah

Katika miaka ya mwanzo ya kutangaza Uislamu, aya hii iliposhuka: "Wa Andhir Ashiiratakal Aqrabiin" – "Na waonye jamaa zako wa karibu" (***As-Shu'araa 26:214***), Mtume Muhammad (s.a.w.w.) alimwita Imam Ali (a.s) na akasema: *"Ewe Ali, Mwenyezi Mungu* (*s.w.t*) *ameniamrisha kuwaita jamaa* (*ndugu*) *zangu wa karibu, hivyo niitie watoto wa* ***Abdulmuttalib*** *na tuandalie chakula kutokana na nyama ya kondoo na maziwa"*.

Imam Ali (a.s) anasimulia kuwa: "Niliwaita kama nilivyoamrishwa na Mtume na walihudhuria takriban watu 40 ikiwa ni pamoja na ami zake Mtume : Abutalib, Hamza, Abbas na Abulahab. Walipokusanyika, Mtume aliwaletea chakula. Ingawa chakula kilikuwa kichache, kiliwatosha kabisa wote waliokuwepo na bado chakula kingine kikabaki.

Baada ya chakula, Mtume alipotaka kuzungumza, Abulahab aliingilia kati na kusema: *"Huyu mwenzenu*

(*Muhammad* (*s.a.w.w.*)*amewaroga",* hivyo watu wakasambaa bila kumsikiliza Mtume. Mtume aliniita tena na kusema: *"Ewe Ali, huyu mtu ameingilia kati na kuzungumza kabla sijazungumza, hivyo waite tena kesho na utuandalie chakula kama leo".*

Siku ya pili walipokuja, Mtume (s.a.w.w.) aliwaletea chakula na walikula wakashiba kama jana yake. Walipomaliza kula Mtume alisimama juu na kuwahutubia: *"Enyi wana wa Abdulmuttalib, kwa hakika Mwenyezi Mungu amenituma kwa watu wote kwa ujumla na kwenu nyinyi niwaite katika Uislamu. Mwenyezi Mungu ameniamrisha kuwa ni waonye ndugu* (*jamaa*) *zangu wa karibu, hivyo ninawaita katika mambo mawili ambayo ni mepesi sana katika ulimi lakini ni mazito sana katika mizani* (*siku ya Kiyama*)*. Mambo hayo ni Shahada ya Laa Ilaaha Illallah na kwamba mimi ni Mtume wa Mwenyezi Mungu. Yeyote atakayezingatia* (*atakayeitikia*) *wito huu na kunisaidia atakuwa ndugu yangu, msaidizi* (*Waziri*) *wangu, Wasii wangu, Mrithi wangu na Khalifa baada yangu*".

Hakuna aliyejibu isipokuwa mimi (Ali bin Abitalib) nilisimama na kusema: *"Mimi Ewe Mtume wa Allah".* Mtume aliniambia nikae chini na akarudia tena maneno yale. Hakuna aliyejibu isipokuwa mimi. "Mimi, Ewe Mtume wa Allah". Mtume aliniambia nikae chini na akarudia maneno yale mara ya tatu. Ilipokuwa hakuna aliyesimama isipokuwa mimi, Mtume aliweka mkono wake katika bega langu na kutangaza: *"Huyu* (*Ali*) *Ni Ndugu Yangu, Wasii Wangu, Waziri* (*Msaidizi*) *Wangu, Mrithi Wangu Na Khalifa Baada Yangu Kwenu, Hivyo Msikilizeni Na Mtiini".*

Wale waliohudhuria waliposikia maneno haya, walisimama juu wakicheka na kumwambia Abutalib: "(Mtume) amekuamrisha umsikilize na umtii mtoto uliyemzaa mwenyewe!"

Huu ni ushahidi na uthibitisho wa kwanza katika ushahidi mwingi uliopo, ambapo Imam Ali bin Abiitalib aliteuliwa kuwa wasiy na Khalifa baada ya Mtume. Hadithi hii inapatikana katika vitabu vifuatavyo vya Kisunni:

– *Taarikh Tabari – Juz. 3, uk. 560*.
– *Sharh Nahjul Balagha cha Ibn Abil Hadiid, Juz. 3, uk. 263*.
– *Al–Kaamil cha Ibn Al–Athiir – Uk. 24.*
– *Taariikh Jawami cha Suyuti*.
– *Musnad cha Imam Ahmad bin Hambal;* na vitabu vingine vingi vya Kissuni.

Kwa sababu hadithi hii ni ushahidi uliodhahiri juu ya Uimamu na Ukhalifa wa Imam Ali bin Abitalib, baadhi ya Maulamaa na waandishi wa vitabu wa Kisunni, wameanza kujaribu kuficha hadithi hii. Moja ya watu waliojaribu kuficha hadithi hii ni Muhammad Husayn Haykal wa Misri. Katika toleo la kwanza la kitabu chake ***"Hayaat Muhammad"*** (Maisha ya Muhammad (s.a.w.w.) iliitaja hadithi kwa urefu wake kama ilivyo ***Hadithi ya Indhaar,*** lakini aliiondoa katika toleo lake pili na la tatu la kitabu hicho hicho kimoja. Kwanini anaamua kuficha ukweli na kujipendelea upande wake? Inashangaza. Qur'an tukufu inasema:

"Na msiufiche ukweli kwa uongo na wala msifiche ukweli na hali mnajua". (***Baqara 2:42***).

Ushahidi / Uthibitisho Na. 2 – Aya Ya Wilayah

Ayatul Wilayah ni aya nyingine ya Qur'an inayothibitisha Ukhalifa wa *Ali bin Abitalib* (a.s) bila shaka yoyote. Aya hii ipo katika *Suratul Maidah* (*5:55*) ambayo inasema:

"Walii wenu ni Allah, Mtume wake na waumini wanaosimamisha sala na wanaotoa zakat ili hali ya kwamba wanarukuu". **(*5:55*).**

Maulamaa wote wa Tafsiir na Hadith, wa Kishia na Kisunni, wanakubali kwamba aya hii iliteremka kwa ajili ya *Imam Ali bin Abitalib* (*a.s*). Baadhi ya mifano ya wasimuliaji wa hadithi wa Kisunni ni kama ifuatayo:

a) Suyuti amesimulia katika tafsiir yake katika kitabu chake ***Tafsiir Durrul Manthur*** kwamba ***Ali bin Abitalib*** alitoa pete yake kama sadaka kwa masikini alipokuwa katika sala akirukuu; hivyo Allah akateremsha aya hii ya Wilayah. (5:55).

b) Mwanazuoni wa Kisuni Tabrani katika kitabu chake ***"Awsat"*** amesimulia kuwa: *"Siku moja maskini mmoja alisimama pembeni ya Ali ambaye alikuwa katika sala akirukuu* (*Sunnah*) *na akaomba chochote, hivyo Ali akampa pete yake kutoka kidole chake alipokuwa katika Rukuu. Mtume* (*s.a.w.w.*) *alipokuja msikitini Imam Ali alimuarifu Mtume juu ya tukio hili na hapo hapo ikashuka aya ya Wilayah.* (*5:55*).

Mtume alisoma aya hii kwa sabaha zake na akasema: *"Man Kuntu Mawlahu Fa Alliyun Mawlahu. Allahumma Waali Man Waalaahu, Wa Aadi Man Aadaahu"*. Yaani: *"Kwa yeyote ambaye mimi ni kiongozi wake, Ali ni kiongozi wake wa kumtawalia mambo yake. Ewe Mwenyezi Mungu, kuwa rafiki wa rafiki yake* (*na Ali*) *na kuwa adui wa yule anayeonyesha uadui kwa Ali".*

c) Fakhruddin Raazi katika Tafsiir yake amesema kuwa ***Abudhar Al-Ghaffari*** alisimulia kuwa: Siku moja Mtume alimuomba Allah kwa kusema:

"Ewe Allah, ndugu yangu Nabii Musa alikuomba kwa kusema kipanue kifua changu, irahisishe kazi yangu na ondoa uzito katika kauli yangu, ili waelewe kile ninachokisema na nipatie Wazir **(*msaidizi*)** ***kutoka katika familia yangu, Haruun ndugu yangu, nizidishie nguvu kupitia kwake na mfanye awe mshirika wangu katika kazi yangu....".*** **(*Taha 20:25-32*).**

"Ewe Allah, mimi ni Muhammad, Mtume wako na mjumbe wako Mpendwa, hivyo ninakuomba ukipanue kifua changu, uirahisishe kazi yangu na unipe Wazir (msaidizi) kutoka katika familia yangu, Ali ndugu yangu na niongezee nguvu kupitia kwake ....".

Abudhar anaendelea kwa kusema : "Wallah, Mtume hakumaliza hata kumaliza dua yake, Jibriil akaja na kuteremsha aya ya Wilayah (5:55) ambapo Ali alitoa pete yake kama sadaka kwa masikini alipokuwa akirukuu".

Maulamaa wengine wa kisunni waliosimulia tukio hili ni *: Al-Ganji Shafii katika Kifayat Al-Talib, Shablanji katika Noorul Absaar, Al-Waahidi katika Asbaabun Nuzul, Zamakhshari katika Tafsirul Kashshaf, Ibn Hajr Asqalani katika Al-Kafi Ash-Shafi, Abubakar Ahmed bin Ali Ar-Razi Al-Hanafi katika Ahkamul Qur'an, Al-Qurtubi Al-Undulusi katika Al-Jami' Li Ahkamil Qur'an, Shahabuddin Al-Aluusi katika Ruuhul Ma'aani, Sibt ibn Al-Jawzi katika Tadhkirah, na waandishi wengine wengi wa Kissuni.*

Watafiti wa ukweli wanatakiwa warejee vitabu hivyo hapo juu ili waupate ukweli kuwa Ali bin Abitalib ni Walii, Imam, Khalifa na Wasii baada ya Mtume kama ilivyo katika aya hii ya Wilaya. (5:55).

Qur'an tukufu inaendelea katika aya inayofuata kwa kusema: ***"Na kwa wale walioukubali Uwalii wa Allah na Mtume wake na wale walioamini*** (*Imam Ali bin Abitalib*), ***basi kwa hakika kundi la Allah*** (*Shia wa Imam Ali*) ***ndio wenye kufaulu".*** (***Maidah 5:56***). Aya hii inafuatia baada tu ya aya ya *Wilaya* (***5:55***).

Kwa bahati mbaya, baadhi ya watu wanakana Uwalii na Ukhalifa wa Imam Ali bin Abitalib (a.s) mara tu baada ya Mtume (s.a.w.w). Juu yao Qur'an inasema : ***"Wanazitambua neema za Allah, kisha wanazikataa, na wengi wao hawana shukrani".*** (***Nahl 16:83***).

Ushahidi / Uthibitisho Na. 3 - Hadith Al-Manzilah

Wanazuoni wote wa Kishia na Kisunni wanakubali juu ya usahihi wa hadithi hii. Mtume Muhammad (s.a.w.w.) alipokwenda katika vita vya Tabuk katika mwaka wa 9 Hijria, alimuacha Imam Ali kama Khalifa wake Madina. Tabuk (katika mpaka wa Syria) ilikuwa ni mbali sana na Mtume alipaswa kumuacha mtu thabiti na mwenye imani kubwa ili kuulinda mji mkuu wa Dola ya Kiislamu Madina, kutokana na uovu wa washirikina, na hususan wanafiki ambao walikuwa wanasubiri wapate nafasi japo ndogo ili walete mtafaruku Madina. Hivyo Mtume alimteua Imam Ali ili awe Khalifa wake katika kipindi hiki ambapo Mtume alikuwa safarini.

Wanafiki walianza kumchokoza *Imam Ali* kuwa hakwenda Jihad ili kuokoa maisha yake na kwamba alikuwa anaogopa kifo. *Imam Ali* hakufurahia maneno haya, hivyo alikwenda kwa Mtume kumuomba aende naye vitani (Jihad). Mtume alijibu kuwa haikuwa vizuri kwake yeye Mtume kuondoka bila kumteua Ali kama Khalifa wake, pale Madina.

Kisha alisema: *"Amaa Tardhaa An Takuuna Minni Bi Manzilati Haaruna Min Musa, Illaa Annahu Laa Nabiyya Ba'dii" - "Je hauridhiki kwamba wewe kwangu una nafasi kama ile aliyokuwa Haruni kwa Musa, isipokuwa tu hakuna Mtume baada yangu?*"

Hadithi hii inathibitisha waziwazi kuwa nafasi ya Ali ni sawa na ile ya Haruni. Sasa tujiulize ni ipi ilikuwa nafasi ya Haruni ? Hebu tuiangalie nafasi ya Haruni katika Qur'an Tukufu.

"Na nipatie Waziri kutoka katika familia yangu, Harun ndugu yangu, na niongezee nguvu kupitia kwake na mfanye awe mshirika katika kazi yangu". (***Taha 20:29-32***).

"----- Na Musa alisema kumwambia ndugu yake Haruun; Kuwa Khalifa wangu miongoni mwa watu wangu ---- ". (***A'araf 7:141***).

Aya hizo hapo juu zinathibitisha kuwa Harun alikuwa ni Ndugu, Waziri, Msaidizi, Khalifa na Mrithi wa Nabii Musa. Halikadhalika kwa mujibu wa *Hadithi Al-Manzilah, Imam Ali ni Ndugu, Wazir, Msaidizi, Khalifa, na Mrithi wa Mtume Muhammad baada yake.* Je, bado tu hamuielewi na kuitii amri ya Mtume Muhammad (s.a.w.w.) enyi Waislamu!

Hadithi ya Manzilah imesimuliwa na mamia ya Wasimuliaji wa hadithi wa Kisunni, baadhi yao ni kama ifuatavyo:

- *Sahih Bukhari, Baab Ghazwat Tabuk, Juz. 3, uk. 54*.
- *Sahih Bukhari, Baab Manaqib Ali Bin Abitalib, Juz. 2, uk. 185.*
- *Sahih Muslim, Baab Fazail Ali, Juz. 2, uk. 236*.
- *Musnad Ahmad bin Hambal, Juz. 1, uk. 98 na uk. 236.*
- *Hakim katika Al-Mustadrak, Juz. 3, uk.109*.
- *Suyuti katika Tarikhul Khulafa, uk. 65.*
- *Ibn Al-Kathir katika Usudul Ghaabah, Juz. 4, uk. 26.*
- *Ibn Hajr Al-Asqalani katika Isaabah, Juz. 2, uk. 507.*
- *An-Nasai katika Khasais, Uk. 7 na Uk. 15.*
- *Taariikh Ibn Asaakir, Juz. 4, Uk. 96 n.k*.

Soma makala Na. 3 kwa ushahidi zaidi juu ya ***Ukhalifa wa Imam Ali bin Abitalib*** (***a.s.***). Qur'an Tukufu inasema:

*"**Na sema: Ukweli sasa umefika** (**umekuja**), **na uongo umeondoka, na daima uongo huwa ni wenye kuondoka**".* (***Bani Israel 17:81***).

Sheikh Muslim Bhanji
Tanzania Ithna Ashariyah Community (T.I.C.)
Dodoma
July 2001

Bismihi Ta'ala
"Na katika haya imekujia Haki na mauidha na ukumbusho kwa wale wanaoamini."(***Suratul Hud 11:120***)

Katika makala yetu Na. 2, tulianza kutoa ushahidi kutoka katika Qur'an Tukufu na vitabu vinavyotambulika vya Ahlul Sunnah Wal Jama'ah kuthibitisha kuwa Mtume Muhammad (s.a.w.w.) alimteua Imam Ali bin Abitalib (a.s) kuwa Wasiy na Khalifa baada yake.

Aidha katika makala Na. 2, tulitoa uthibitisho wa aina tatu juu ya hilo, na ushahidi huo ni: (1) *Hadithi Indhar au Da'wat Dhul Ashirah.* (*2*) *Aya ya Wilayah.* (*3*) *Hadithi ya Manzilah.* Katika makala hii Na. 3 na zitakazofuatia, tutatoa ushahidi zaidi kuthibitisha Uimamu wa Ali bin Abitalib (a.s).

Ushahidi Na. 4 – Hadithi Ya Thaqalayn Quran Na Ahlul Bayt

Katika Hadithi hii ya Thaqalain, Mtume Muhammad (s.a.w.w.) ameripotiwa akisema:
"Innii Taarikun Fiikum Al-Thaqalayn: Kitaballahi Wa Itratii Ahlu Baytii, Maa In Tamassaktum Bihimaa Lan Tadhillu Ba'dii Abadan".

"Ninawaachieni vitu viwili vizito, kitabu cha Mwenyezi Mungu (*Qur'an Tukufu*) *na kizazi changu Ahlul Bayt, na ikiwa mtashikamana na hivi vitu viwili, basi kamwe hamtopotea".*

Hadithi hii inathibitisha waziwazi kuwa, kabla ya kufariki, Mtume alituachia Ahlul Bayt kama viongozi wetu na Imam Ali (a.s) alikuwa ni kiongozi wa Ahlul Bayt baada ya Mtume Muhammad (s.a.w.w.), hivyo Imam Ali ni Khalifa wa Waislamu baada ya Mtume.

Hadithi ya Thaqalayn imesimuliwa na vitabu vyote vikubwa vya Ahlul Sunnah Wal Jama'ah na ambayo inachukuliwa kuwa ni hadithi sahihi kabisa kuliko zote na Maulamaa wote wa Kisunni, peke yake tu ni ushahidi tosha na ni uthibitisho wenye uzito kabisa unaothibitisha Uimamu wa Ali bin Abitalib (a.s) baada ya Mtume Muhammad (s.a.w.w.).

Imekubaliwa pia na maulama wa Kisunni kuwa hadithi hii imeelezwa na Mtume, sio mara moja bali katika maeneo na matukio mbalimbali kiasi kwamba hadithi hii imekuwa maarufu na imesimuliwa na mamia ya wanahadithi (wapokezi wa hadithi).

Katika moja ya matukio ambapo Mtume aliitoa hadithi hii ilikuwa ni katika viwanja vya Arafati wakati wa Hajjatul Widaa' (Hijja ya Mwisho ya Mtume), Siku ya Ghadir Khum – Mtume alipokuwa anarudi kutoka katika Hajjatul Widaa', katika siku zake za mwisho za ugonjwa wake, na katika khutba zake katika mji wa Madina, n.k.

Baadhi ya vitabu vikubwa vya Kisunni vilivyopokea hadithi hii ni hivi vifuatavyo:
1) *Musnad Ahmad bin Hambal, Jz. 3, Uk.17*

2) *Sahihi Muslim, Juz. 2, Uk. 237.*

3) *Kanzul Ummal, Juz. 7, Uk. 112.*

4) *Sahihi Tirmidhi, Juz. 2, Uk. 308*.

5) *Mustadrak Al-Hakim, Juz. 3,Uk. 109.*

6) *Yanaabi ul Mawaddah, Uk. 25*.

7) *Tafsiir Ibn Kathiir, Juz. 3, Uk. 486.*

8) *Sawa'iq Al-Muhriqah, Uk. 150.*

9) *Taarikh Al-Ya'quubi, Juz. 2, Uk. 93*

10) *Dhakhair Al-Uqba cha Tabari, Uk. 16.*

Na vitabu vingenevyo vingi ambavyo hatutavitaja hapa kwa sababu ya uchache wa nafasi.

Imam Suyuti amesimulia katika kitabu chake: *Ihyaa'ul Mayyit,* kwamba katika maradhi ya mwisho ya Mtume (s.a.w.w.), Mtume aliwahutubia sahaba zake kwa kusema: *"Enyi watu, ninakaribia kuondoka duniani kwenda kuonana na Mola wangu Mtukufu, lakini kuweni makini, ninawaachia vitu viwili: Kitabu cha Allah na kizazi changu Ahlul Bayt".* Kisha aliunyanyua na mkono wa Imam Ali (a.s) na kusema:

"*Haadha Ali Ma'al Qur'an, Wal Qur'anu Ma'a Ali, Laa Yaftariqaani Hattaa Yaridaa Alayyal Hawdh." – "Huyu Ali yuko pamoja na Qur'an na Qur'an iko pamoja na Ali, na kamwe hawatoachana mpaka watakaponikuta katika chemchem* (*Hawdhi*) *za Kawthar".*

Mtume alituachia Qur'an na *Ahlul Bayt* ili tuvishikilie vitu hivi viwili kwa nguvu, ili tusipotee na tumkute Mtume Peponi katika chemchem za Kawthar kwa mafanikio. Lakini kwa bahati mbaya baada ya kifo cha Mtume, watu waliwapuuza Ahlul Bayt na wakaiepuka njia iliyonyooka. Najiuliza nini litakuwa jibu lao watakapo kutana na Mtume siku ya Hukumu? Mtume ameiita Qur'an na Ahlul Bayt kama '*Thaqalayn'* (Vitu viwili muhimu na vizito) lakini watu wamevichukulia kiuepesi tu. Tunamuomba Allah atuepushe kutokana na upotovu na dhulma dhidi ya Ahlul Bayt. Amin.

Na la kushangaza zaidi ni ukweli kwamba ingawa Hadithi hii ya Thaqalayn ipo katika vitabu vyote vya Kisunni vinavyo tambuliwa, lakini bado baadhi ya Maulama wa Kisunni wanajaribu kuuficha kwa sababu wanazozijua wenyewe au ili kuwadanganya wafuasi wao ambao hawajasoma vya kutosha, kuwa hadithi hii inapatikana katika vitabu vya Shia tu.

Kuna kipindi niliwahi kualikwa ili nitoe mada / hotuba juu ya umuhimu wa elimu katika moja ya misikiti ya Sunni, Dodoma. Ili kuonyesha elimu walivyokuwa nayo Ahlul Bayt, niliitoa Hadithi ya Thaqalayn katika hotuba yangu. Baada ya Majlis (Mkutano), ndugu yetu mmoja Mwislamu Sunni alialikwa kufunga kikao kwa dua. Yule ndugu yetu alijifanya kuwa ni mwanazuoni mkubwa na Ahlul Sunnah na badala ya kufunga kikao tu kwa dua' kama alivyotakiwa kufanya, aliuonyesha wazi ujinga wake / kutokujua kwake na alionyesha uadui wake dhidi ya wafuasi wa Ahlul Bayt, kabla ya dua alisema: "Hadithi ya Thaqalayn, vitu vizito viwili: Qur'an na Ahlul Bayt haipo kabisa katika vitabu vya Kisunni na hadithi hii sio sahihi". Uongo gani mkubwa huu dhidi ya Mwenyezi Mungu na Mtume wake!

Baadaye, baada ya kikao nilimfuata na kumwambia kuwa nina vitabu vingi vikubwa vya Kisunni kama Sahihi Muslim, Musnad Ahmad, Riyadhus Swaliheen, n.k. ambamo hadithi imepokelewa na kuandikwa, na nilimwalika aje kwangu ili nimpe ushahidi, lakini hakuthubutu kutokea. Nilitoa vivuli (photocopy) vya

kurasa za vitabu hivi ambamo hadithi imetajwa na nikamtumia, lakini hakujibu wala hakuonyesha kujuta kwa kitendo chake cha kuikana hadithi ambayo ipo katika vitabu vyake. Tunamuomba Mwenyezi Mungu amuongoze katika njia iliyonyooka – Amin.

Ahlul Bait Ni Akina Nani?

Swali muhimu kabisa ambalo tungependa kulijibu sasa ni Ahlul Bait ni akina nani? Au Ahlul Bait ni wepi? Hapa pia tutatoa majibu kutoka katika vitabu vya Sunni tu.

1) Muslim anasimulia katika Sahihi yake kutoka kwa Safiya bint Shaibah ambaye aliripoti kuwa: "Siku moja Aisha bint Abubakar alisema: "Siku moja Mtume wa Allah alikuwa amejifunika Kisaa (blanket kubwa), kisha akaja Imam Hasan (a.s) na Mtume akamuita na kumfunika na Kisaa. Kisha akaja Imam Husayn (a.s) na pia Mtume akamfunika. Kisha akaja Fatima (a.s) na Mtume akamfunika kwa Kisaa. Kisha akaja Imam Ali (a.s) na Mtume pia akamfunika kwa Kisaa. Kisha akasema:

"Innamaa Yuriidullahu Liyudh'hiba Ankumur Rijsa Ahlal Bayti, Wa Yutahhirakum Tat-hiira". – "Mwenyezi Mungu anataka kukuondoleeni uchafu enyi Ahlul Bayt na anataka kukutakaseni utakaso ulio bora kabisa". (***Suratul Ahzab 33:33***).

Hadithi hii inaonyesha waziwazi kuwa **Ali, Fatima, Hasan na Husayn** ndio Ahlul Bayt wa Mtume Muhammad (s.a.w.w.) ambao wameteuliwa na Mtume kuwa viongozi wetu. (*Angalia Sahih Muslim, Jz. 5, Uk. 287*).

2) Katika Sahihi Muslim imeripotiwa kuwa: "Aya ifuatayo iliposhuka: ***"Na atakayebishana nawe baada ya kukujia elimu, mwambie: Tuwaite watoto wetu na watoto wenu, wanawake wetu na wanawake wenu, na nafsi zetu na nafsi zenu, na kisha tuombe kwa unyenyekevu laana ya Mwenyezi Mungu iwashukie waongo*** (***Aya ya Mubahilah, Aali Imran 3:61***)***;*** *Mtume aliwaiita Ali, Fatima, Hasan, Na Husayn na akasema: "Allahumaa Haa'ulaai Ahlii" – Ewe Mwenyezi hawa ndio watu wa nyumbani kwangu, Ahlul Bayt".* (*Tazama Sahih Muslim, Jz. 5, Uk. 268*).

3) Ingawa Mtume alieleza mara nyingi kuwa Ahlul Bayt ni Ali, Fatima, Hasan, na Husayn; na hii imerekodiwa katika vitabu vingi vya Kisunni na wapokeaji thabiti, lakini utakuta baadhi ya wanazuoni wa Kisunni wanajaribu kung'ang'aniza kuwa Ahlul Bayt ni wake za Mtume.

Ukweli ni kwamba wake za Mtume hawamo katika kundi la Ahlul Bayt, kwa sababu Ahlul Bayt kwa mujibu wa Qur'an ni Ma'asumu (hawana madhambi) na walikuwa wametakasika ambapo wake za Mtume hawakuwa Ma'asumu. Mjadala juu ya mada hii utajadiliwa baadaye. Kwa wale wanaoamini kuwa wake za Mtume ni katika Ahlul Bayt wasome hadithi ifuatayo katika Sahih Muslim, *Juz.5, Uk. 274*.

Muslim amesimulia katika Sahih yake kupitia kwa Zaid bin Arqam ambaye alisema kuwa: "Mtume Muhammad (s.a.w.w.) amesema: *"Enyi watu! jueni kwamba mimi ni mwanaadamu na Malaika wa Mauti anaweza kunijia hata mimi pia na lazima niitike wito wake. Enyi watu! ninawaachieni vitu vizito* (*muhimu*)

viwili; cha kwanza ni kitabu cha Mwenyezi Mungu, ambapo ndani yake mtapata mwongozo na nuru, hivyo shikamaneni na kitabu cha Mwenyezi Mungu na kamwe msikiache; na kizito cha pili ni Ahlul Bayt wangu, ninawakumbusheni juu ya wajibu wenu kwa Ahlul Bayt --- ninawakumbusheni juu ya wajibu wenu kwa Ahlul Bayt ---- ninawakumbusheni juu ya wajibu wenu kwa Ahlul Bayt (alirudia mara tatu)".

Kisha tuliuliza: ***"Ahlul Bayt ni akina nani, Je, wake?"*** *Akasema:* ***"Hapana****. Ninaapa kwa jina la Allah, kwa hakika mwanamke huishi na mumewe kwa muda, kisha mumewe akimpa talaka, hurudi kwa baba yake na jamii yake, Ahlul Bayt ni watu wake kutoka katika familia yake na ambao kwao sadaka ni haramu baada yake". (Sahih Muslim, Baab Fadhail Ali (a.s), Juz. 5, Uk. 274).*

4) Katika Sahih Tirmidhi imeripotiwa kutoka kwa Umru bin Abi Salama ambaye amesema: "Aya hii iliposhuka: ***"Innama Yuridullahu Liyudh Hiba Ankumur Rijsa Ahlal Bayti Wa Yutahhirukum Tat-Hiira"*** *- "Kwa hakika, Mwenyezi Mungu anataka kuwaondeleeni kila aina ya uchafu, enyi Ahlul Bayt, na kuwatakasani kwa utakaso ulio bora kabisa* (***33:33***)", *katika nyumba ya Ummu Salma, Mke wa Mtume; Mtume aliwaita Fatima, Hasan, Husayn na Ali na aliwafunika kwa Kisaa (blanketi); kisha akasema : "Ee Mwenyezi Mungu! hawa ni Ahlul Bayt wangu, hivyo waondolee kila aina ya uchafu na watwaharishe kwa tohara iliyo bora kabisa".*

Ummu Salma akasema: *"Je, na mimi ni pamoja nao (Ahlul Bait) Ewe Mtume wa Allah?" Mtume alijibu: "Hapana, wewe una nafasi yako na upo katika njia iliyonyooka".* Alikataliwa kuingia! Hadithi hii pia imo katika Musnad Ahmad bin Hambal (Juz 6, Uk. 306), na Sahih Tirmidhi (Juz. 2, Uk. 209).

5) Katika aya ya Tathiir: ***"Innamaa Yuridullahu Liyudh-Hiba Ankumur-Rijsa Ahlal Bayti Wa Yutahhirakum Tat-Hiira*** (***Ahzab 33:33***)**,** dhamiri ya Kiarabu iliyotumika kwa Ahlul Bayt ni "***Ankum……, Yutahhirukum***....". Wakati katika sura hiyo hiyo katika aya zilizotangulia (***Ahzab 33:32-34***) dhamiri iliyotumika kwa wake za Mtume ni "***Kuntunnaa….., Minkunna……., n.k."*** ambayo ni dhamiri ya kike kwa kiarabu.

Badiliko hili la ghafla la dhamiri kutoka dhamiri ya kike kwenda dhamiri ya kiume katika Aya (***Ahzab 33:33***)**,** inathibitisha kuwa wake za Mtume hawamo katika Ahlul Bayt ambao wanatakiwa kufuatwa, kwa sababu wakati Mwenyezi Mungu (s.w.t.) alipotaka kuwazungumzia wake za Mtume alitumia dhamiri ya kike ***"Kuntunna ….., Minkunna……",*** lakini alipoanza kuwazungumzia Ahlul Bayt ***"Ali, Fatima, Hasan na Husayn"****,* dhamiri ilibadilika. Huu ni ushindi dhahiri kwa wale wanaojua sarufi ya lugha ya Kiarabu.

Wapendwa wasomaji, mmeona kwamba hadithi ya ***Thaqalayn*** (***vizito viwili***) ***: Qur'an na Ahlul Bayt*** imeripotiwa katika vitabu vingi sana vya Kisunni, lakini umewahi kumsikia mwanazuoni wa Kissuni akiizungumzia hadithi hii - Kushikamana na Qur'an na Ahlul Bayt - ambao ndio ulikuwa wasiyya wa mwisho wa Mtume. Kwanini wanazuoni wa Kisunni wanaupuuza wosia wa mpendwa kiongozi na Mtume wetu? Je, kuna sababu yoyote ya maana ya kuupuza wosia huu (jambo ambalo ni dhambi kubwa) zaidi ya kuwa ni ujinga, ugumu wa mioyo, kujiegemeza upande wa imani zetu ulizonazo, wivu na manufaa yetu binafsi? Tunamuomba Mwenyezi Mungu atupe tawfiiq ya kushikamana na Qur'an na Ahlul Bayt

baada ya Mtume (s.a.w.w.) Amin.

Ushahidi Na. 5 – Hadithi Ya Safina / Jahazi

Katika kitabu cha Kisunni: Mustadrak Sahihein imesimuliwa na Hakim kupitia kwa Hanash Al–Kanani ambaye alisema: Nimemsikia Abudhar Al–Ghafari akisema wakati alikuwa ameushika mlango wa Kaa'ba Tukufu: "Enyi watu, wale wanaojua mimi ni nani wananijua, lakini wale wasionijua na wajue kuwa mimi ni Abudhar (Sahaba wa Mtume). Nimemsikia Mtume (s.a.w.w.) akisema:

"Mathalu Ahlulbaytii Fiikum Mathali Safiinatin Nuuh, Man Rakibaha Najaa, Wa Man Takhallafa Anha Gharika". – *"Mfano wa Ahlul Bayt wangu ni kama Safina / Jahazi ya Nuuh (a.s). Kila aliyeipanda aliokoka, na kila aliyejiepusha nayo aligharikishwa".* Mwanachuoni wa Kisunni Hakim amesema kwamba hadithi hii ni Sahihi.

Pia hadithi hii ya Safina imesimuliwa na mamia ya wanazuoni wa Kisunni katika vitabu vyao. Umewahi kumsikia mwanazuoni yeyote wa Kisunni akiizungumzia hadithi hii kwenye hotuba yake? Kama hujawahi, basi wanazuoni hao wanaificha. Lakini unaweza kurejea vitabu vifuatavyo vya Kisunni na utaipata hadithi hii:

● *Al–Hakim katika Mustadrak yake, Juz. 2, Uk. 343.*

● *Sawaiq Muhriqah, Uk. 153.*

● *Faraid Simtein, Juz.4,Uk. 149.*

● *Mustadrak Sahihein, Juz.3, Uk. 343.*

● *Nuural Absaar, Uk. 126;* na vitabu vingine vingi.

Waislamu waliotaka kunusurika na moto wa Jahannamu siku ya Kiyama waliwafuata AhlulBayt – Imam Ali (a.s), baada ya kuondoka kwa Mtume. Ni sababu gani inayotufanya tusiwafuate Ahlul Bayt baada ya Mtume na hali ya kuwa Ahlul Bayt ni safina ya Nuuh (a.s)?

Kwa hakika, hatutaki kuwa kama mtoto wa Nuuh (a.s) ambaye juu yake Qur'an inasema:

" ---- na Nuuh alimwita mwanae, na alikuwa peke yake. Ewe mwanangu! ingia (ndani ya Safina) uwe pamoja nasi na usiwe miongoni mwa makafiri (wasio amini). Alisema nitakimbilia mlimani, mlima ambao utanilinda dhidi ya maji. Nuuh akasema hakuna mlinzi leo atakayekulinda dhidi ya adhabu ya Mwenyezi Mungu isipokuwa yule mwenyewe kurehemewa. Kisha wimbi likapita kati yao, hivyo akawa ni miongoni mwa waliogharikishwa". (Huud 11:41–43).

Ni nani atakayetuokoa dhidi ya gharika ikiwa hatutoingia katika jahazi / safina ya Ahlul Bayt? Tunamuomba Allah (s.w.t) atunusuru na gharika tusiwe kama alivyokuwa mtoto wa Nuuh. Amin.

Ushahidi Na. 6 – Hadithi Nyingine Juu Ya Ahlul Bayt

Kuna hadithi nyingi sana za Mtume Muhammad (s.a.w.w.) zinazoonyesha fadhail na uongozi wa Ahlul Bayt (a.s). Tutatoa hadithi chache hapa chini kutoka katika vitabu vya Kisunni ili kuthibitisha nafasi ya Ahlul Bayt baada ya Mtume Muhammad (s.a.w.w.):

1) Ibn Abbas amesimulia kwamba Mtume Muhammad (s.a.w.w.) kasema: *"Nyota huwaongoza watu wa dunia ili wasiangamie. Hali kadhalika Ahlul Bayt wangu ni viongozi wa Ummah wangu watakaouepusha ummah wangu kutokana na utengano na kutofautiana* (*kuhitilafiana*)*; na yeyote miongoni mwa makabila ya kiarabu atakayewapinga, atakuwa ni kutoka katika kundi la Iblis".* (*Mustadrak Sahihein, Juz .2, Uk. 343; Sawaiq Al–Muhriqah, Uk. 235*).

Ingekuwa waqureishi walikubaliana juu ya Uimamu wa Ali bin Abitalib (a.s) na wangekuwa hawakumpinga Mtume (s.a.w.w.) juu ya suala hili, Ummah wa Kiislamu ungekuwa umeepukana na Utengano na Khitilafu. Lakini kwa bahati mbaya ukhalifa wa Ali (a.s) ulinyang'anywa, na Ahlul Bayt walipingwa.

2) ***Jinsi ya Kumsalia Mtume (s.a.w.w.) – Salawat*** – Mtume Muhammad (s.a.w.w.) amewaelekeza waislamu kuwajumuisha Ahlul Bayt wake (Aali Muhammad) wakati wa kumtumia salawat, na hairuhusiwi kuiondoa Aali Muhammad kwenye Salawat.

Kwenye Sahih Bukhari, imetajwa kwamba siku moja masahaba walimuuliza Mtume Muhammad (s.a.w.w.): *"Ewe Mtume wa Allah, tumeelewa jinsi ya kukusalimia, lakini tufundishe jinsi ya kukutumia salawat* (*kumsalia Mtume*)*". Alijibu: "Semeni Allahumma Swalli Alaa Muhammad Wa Alaa Aali Muhammad, Kama Swallayta Alaa Ibrahim Wa Alaa Aali Ibrahim, Innaka Hamidun Majid.* (*Sahihi Bukhari, Juz.8, Uk. 245*).

Swali hili liliulizwa na masahaba baada ya amri ya salawat kuteremka katika Qur'an: ***"Innallaha Wa Malaaikatahu Yusalluna Alan Nabii. Yaa Ayyuhal Ladhiina Aamanu Swallu Alaihi Wa Sallimu Tasliima"*** – *"Kwa hakika Mwenyezi Mungu na malaika wake wanamtakia rehema Mtume. Enyi mlioamini! Mtakieni rehema Mtume na msalieni"*. (***Ahzab 33:56***).

Maulamaa wa Kisunni na wa Kishia wamekubaliana kuwa aya hii ilishuka kwa ajili ya fadhail za Mtume na Ahlul bayt wake. Rejea vitabu vifuatavyo vya Kisunni:

1– *Asbabun Nuzul cha Wahidi,Uk. 271*.

2– *Al–Mustadrak cha Hakim, Juz. 3, Uk. 148.*

3– *Tafsiir Fakhruddin Raazi, Juz. 25, Uk. 226.*

4– *Riyadhu Swalihun cha Nawawi, Uk. 4555*

5– *Jami' Li Ahkamil Qur'an cha Qurtubi, Juz. 14, Uk. 233–34.*

Imesimuliwa katika Sawaiq Al–Muhriqah cha mwanazuoni wa Kisunni *Ibn Hajar* (Uk. 144) kwamba: *Mtume Muhammad* (*s.a.w.w.*) *alisema: "Msiifupishe salawat* (*salawat Al–Bataraa*)*". Baada ya kuulizwa nini itakuwa ufupisho wa salawat?* Mtume (s.a.w.w.) alijibu: *"Mnaposema : Allahuma swalli alaa Muhammad* – na mkaishia hapa, hii haitosihi, lazima mseme: ***Allahumma swalli alaa Muhammad wa Aali Muhammad***."

Kwa bahati mbaya ndugu zetu wa Kisunni wanapotuma salawat, wanajiepusha kusema Aali Muhammad, hivyo wanatoa salawat isiyotimia na wanakhalifu maelekezo ya Mtume. Kwa mfano katika mawaidha au majlis, wasikilizaji wa Kisunni, kwa kawaida wanaposikia jina la Mtume humtumia salawat isiyokamili kwa kusema *Allahumma Swalli Wa Sallim Alaihi, bila kusema Wa Aalihi.* Hata maulamaa wa Kisunni wanapoandika jina la Mtume wanaandika salawat isiyotimia *Swallallahu Alaihi Wassallim;* wanaondoa *"Wa Aalihi".* Je, ni ujinga au wivu, au kujiegeamiza upande wao / kujipendelea hata kama sio sahihi au nini, nashangaa?

Katika hadithi nyingine, Mtume Muhammad (s.a.w.w.) alisema: *"Yeyote atakaye sali sala na ndani ya sala yake asinisalie mimi na Ahlulbayt wangu, sala yake haitokubaliwa".* (*Tazama : Shifaa ya Qaadhi Ayadh Maghrabi Juz. 2, Uk. 55; Sawaiq Al–Muhriqa cha Ibn Hajar Uk. 139*).

Mwanachuoni wa Kisunni Raazi katika Tafsiri yake (Juz.7, Uk. 391) ametaja Ahlulbayt ni sawa na Mtume katika mambo matano: (***1***) ***Salawat*** (***2***) ***Salamu*** (***3***) ***Tahara yaani Ismah*** (***4***) ***Sadaka kwao ni haramu*** (***5***) ***Kuwapenda ni wajibu.***

Imam Shafii amesema katika shairi lake maarufu kuwasifu Ahlulbayt: *"Ahlulbayt wa Mtume, kuwapenda nyinyi ni wajibu kwa kila mwislamu kama ilivyofunuliwa kwenye Qur'an. Hii ni fadhail kubwa sana kiasi kwamba kwa yeyote ambaye hatowatumia salawat, sala yake inakuwa batili".*

3) **Aya ya Mawaddah** – ***"Qul Laa As'alukum Alaihi Ajran Illal Mawaddata Fil Qurba".*** – *"Sema siwaombi ujira isipokuwa kuwapenda jamaa zangu wa karibu".* (***Shura 42:23***).

Tafsiri zote na vitabu vya hadithi kwa pamoja vinasema kuwa Ahlulbayt na Qurba hapa ni Ali, Fatima, Hasan na Husayn, na kuwapenda ni wajibu kwa kila mwislamu kwa sababu iliposhuka aya hii Mtume aliulizwa: *"Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu! Ni nani hao jamaa zako wa karibu* (*Qurba*) *ambao kuwapenda imekuwa ni wajibu kwa kila mwislamu? Mtume alijibu:* ***"Ni Ali, Fatima na watoto wao wawili Hasan na Husayn"***.

Tazama :
1. Sahih Bukhari, Juz. 6, Uk. 129.
2. Tafsiir Tabari, Juz. 25, Uk. 14.
3. Tafsiir Al–Kasshaf, Juz. 3, Uk. 402.
4, *Tafsiir Al–Waadhih , Juz. 25, Uk. 19.*

Aya hii ya Mawaddah iliposhuka (42:23), baadhi ya watu walianza kuwaza akilini mwao kuwa Mtume anataka tuwapende Ahlulbayt wake kwa matakwa yake mwenyewe. Hivyo Jibril alikuja na kumwambia Mtume. Baadhi ya watu wanakulaumu kwa upendeleo. Hivyo aya hii ikashuka: ***"Je mnasema ameitunga Qur'an?"*** (***Shura 42:24***).

Alhamdulillah, sisi Shia Ithna Ashariyah tunawapenda Ahlulbayt, na tunawapa nafasi wanayostahili, tunawafanyia Maulid kila mmoja wao, tunafurahia furaha zao na hatuzifurahii huzuni zao, na tunaamini kuwa wao ni viongozi wetu baada ya Mtume (s.a.w.w.). Tunawaita Waislamu wote kujiunga nasi katika kuwafuata Ahlulbayt baada ya Mtume.

Qur'an inasema katika aya hiyo hiyo ya Mawaddah : ***"Na yeyote atakayechuma wema*** (***kwa kuwapenda Ahlulbayt***) ***tutamzidishia wema, kwa hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye kusamehe, Mwenye shukrani*** (***Shura 42:23***). (*Tafsiir Baghawi na Tafsiir Tha'labi*). Soma makala Na. 4 kwa ushahidi zaidi juu ya ***Ukhalifa wa Imam Ali bin Abitalib*** (***a.s***).

Wa Billahi Tawfeeq.

Sheikh Muslim Bhanji,
Tanzania Ithna Ashariyah Community (**T.I.C.**),
Dodoma,
August 2001.

Source URL: https://www.al-islam.org/wito-kwa-waislamu-kuuendea-ukweli-shaykh-muslim-bhanji

Links
[1] https://www.al-islam.org/user/login?destination=node/44941%23comment-form
[2] https://www.al-islam.org/user/register?destination=node/44941%23comment-form
[3] https://www.al-islam.org/person/shaykh-muslim-bhanji-0
[4] https://www.al-islam.org/library/imam-ali
[5] https://www.al-islam.org/library/sunni-shia
[6] https://www.al-islam.org/library/hadith-sciences
[7] https://www.al-islam.org/feature/shia-beliefs-explained